

Toa Kwa Ukarimu

Mtume Paulo, mfuasi wa nguvu wa Yesu, alianzisha kanisa kule Makedonia. Lilikuwa kanisa lililokuwa na watu walioishi kwa 'Umaskini uliokithiri'. Hawako peke yao. Kuna watu masikini wengi ambao wamemfuata Yesu kwa Karne nyingi. Wamakedonia walikumbana na shida nyingi na hawakuwa na mali au pesa nyingi. Pia walikuwa wakarimu sana. Katika Wakorintho 8:1-7 tunasoma kuwahuu na hadithi yao ya kulisimua.

Wamakedonia walikuwa wakarimu zaidi ya vile walivyotarajiwa kuwa Hawakutoa tu vitu vyao vya ziada au vile vilivyokuwa rahisi kwao. Kumbuka kwamba walikuwa masikini hohe hahe huku watu wengi wakiteseka. Walikuwa na shauku ya kutoa. Ndiposa Paulo anawapongeza kama mfano katika kutoa. Hivi ndivyo Paulo alivyosema kuwahuu: "Nashuhudia kuwa walitoa kwa kadri walivyoweza na hata kupita uwezo wao. Kibinafsi wao wenyewe, kwa haraka walitusihi kuwapa fursa ya kushiriki huduma hii kwa watu wa Mungu."

Inaonekana kama kinyume kimawazo! Ni kama walisema, 'Sisi ni masikini na hatuna vya kutosha basi wacha tuwape wengine.' Kwa nini walifanya hivi? Kifungu kinasema, "Furaha yao kuu na umaskini wao uliokithiri uliongezeka kuwa ukarimu mkuu." Walikuwa na imani kuu na kuamini Mungu kiasi cha kuwawezesha kuwa na upendo mkuu kwa wengine na kutoa kwa ukarimu licha ya umaskini uliokithiri. Waliwahesabu wengine kama waliostahili fedha zao kuliko wao wenyewe. Ni mara ngapi tunawaza hivyo?

Ukweli wa ajabu kuhusu kifungu hiki ni kuwa sote, tuwe maskini au matajiri, tunapaswa kumwabudu Mungu pamoja na ukarimu wetu. Kifungu hiki si kuhusu mtu mmoja anayetoa peke yake, bali ni kuhusu kundi la waumini wakitoa kwa pamoja. Mara nyingi ni vigumu kufanya jambo kibinafsi. Labda unafikiria, "Kuna haja gani ya kutoa ilhali naweza kutoa kiwango kidogo tu?" Kwa pamoja tunaweza kufanya mambo makuu. Tukiweka vipawa vyetu pamoja na vya wengine hicho kidogo kitakuwa kikubwa. Hiyo ndiyo nguvu ya ukarimu wa Kikundi. Ni rahisi kutazama hali zetu, ambazo ni chochote kile, na tuamue ikiwa tutaweza au hatutaweza kuwapa wengine. Je naweza kuwahimiza tuwe wakarimu kwa wengine kwa pamoja kama kanisa la Makedonia?

Zingatia!

Jambo kubwa kuhusu ukarimu ni kuwa tunaweza kuanza mahali tulipo! Na kikundi chako au kikundi cha marafiki, tuamue pamoja kuwasaidia watu walio maskini kuliko sisi kama Kanisa la Makedonia. Kwa nini tusikusanye fedha, chakula, au kwa ya wale watu wa kiwango cha chini katika Kijiji chenu au katika Jamii? Mnaweza kupeana mavazi, wakati, kwa hakika, almuradi kinakugarimu na unakipeana kwa ukarimu. Chochote ambacho unaweza kupeana kinaweza kuwa cha msaada mkubwa.


Omba:

- 1) Mungua atachukua kipawa unachotoa na kukizidisha ili kuwabariki wale unaowapa.
- 2) Unapotoa utatambua furaha inayomiminika!



-Mchungaji Esau* alihudhuria mafunzo ya Kikundi cha Maisha hivi karibuni. Alifurahishwa na kile alichosikia na akatoa N\$120 (Pauni 6) kwa hayo. Mchungaji angeweza kutumia fedha hizo kushughulikia mahitaji mengine mengi, ila aliamua kubariki kazi hiyo na kuwasaidia wengine kujifunza kuhusu Vikundi vya Maisha, akiwekeza katika Jamii yake.

- Mchungaji Esau,* Yinsu, Namibia



Funzo hili limechochewa na "Toa kama Kanisa la Makedonia" funzokutoka Penda Kijiji Chako.

Kwa zaidi:

dignityonline.org.uk/publications